



OR-TAMISEMI

TAMISEMI HABARI

TOLEO LA 1

Feb-April, 2019



**Waziri Jafo Awataka
Wakuu Wa Mikoa Kuwasilisha Majina ya
Shule Ambazo Hazijasajiliwa**

WAKUU WA MIKOA WATAKIWA KUWASILISHA MAJINA YA SHULE AMBAZO HAZIJASAJILIWA

Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala wa Mikoa wametakiwa kuorodhesha na kuwasilisha majina ya shule ambazo hazijasajiliwa ili shule hizo zisajiliwe na kutoa fursa kwa wanafunzi wengi kujiunga na shule za umma kwa mwaka wa masomo 2019.

Aidha, Waziri wa Nchi OR-TAMISEMI Mhe. Selemani Jafo amesema wamebaini ubadhirifu wa jumla ya Sh bilioni 7.63 katika halmashauri tano nchini.

Akizungumza wakati akifunga mafunzo kwa Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala wa Mikoa yaliyoandaliwa na Taasisi ya Uongozi, Jafo alisema: "Leteni orodha ya shule ambazo bado hazijapata usajili ili tuzungumze na wenzetu wa elimu, lengo ni kuhakikisha vijana wengi wanaingia katika shule za umma."

Aidha, kuhusu fedha zilizotafunwa katika halmashauri hizo, Jafo alisema kuwa fedha hizo ni za miradi ya maendeleo.

"Nandeni mkatekeleze majukumu yenu kwa kuzingatia sheria lakini msione aibu kwa watu waliofanya ubadhirifu katika maeneo yenu muwachukulie hatua. Haiwezekani image (taswira) yenu inaharibika," alisema.

Akitolea mfano namna ambavyo baadhi ya watendaji wamefanya ubadhilifu, Jafo alisema Halmashauri ya Nyang'wale ambayo kwa mara ya kwanza iligundulika kuwa na ubadhilifu wa Sh bilioni 2.2 baada ya kutuma timu ya ukaguzi kwa mara ya pili wamegundua ubadhirifu wa Sh bilioni 3.9.

Alizitaja halmashauri nyingine ambazo fedha zimeibiwa licha ya Nyang'wale kuwa ni Meru Sh bilioni 1.5, Mbulu zaidi ya Sh milioni 24, Kibaha Mji zaidi ya Sh milioni 22 na Ulanga Sh bilioni 2.04.

"Nawapa picha hii mfahamu kwamba kuna kazi kubwa sana ya kufanya katika maeneo yenu kama haya yanatokea na sisi tupo huoni kama kuna mahali hatujasimamia ipasavyo

Inaendelea Uk...14



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI Mhe. Selemani Jafo akizungumza wakati wa kufunga mafunzo ya Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala



Baadhi ya Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala wakimkiliza mgeni rasmi Mhe. Selemani Jafo (hayuyupo pichani) wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya Uongozi.

SIRI YA MAFANIKIO OFISI YA RAIS TAMISEMI



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI
Mhe. Selemani Jafo (Mb)



Naibu Waziri OR- TAMISEMI
Mhe. Waitara Mwita (Mb)



Naibu Waziri OR-TAMISEMI
Mhe. Josephat S. Kandege (Mb)



Katibu Mkuu OR-TAMISEMI
Eng. Joseph Nyamhanga



Naibu Katibu Mkuu OR-TAMISEMI
Tixon Nzunda



Naibu Katibu Mkuu OR-TAMISEMI
Dkt. Dorothy Gwajima

MHANDISI IYOMBE ATUNUKIWA TUZO YA UTUMISHI ULIOTUKUKA

Shirika la maendeleo la Japan (JICA) limemtunuku aliyekuwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais TAMISEMI Mhandishi Musa Iyombe Tuzo ya Umahiri na Utumishi Uliotukuka.

Akizungumza katika hafla ya kukabidhi Tuzo Mwakilishi Mkuu wa JICA Tanzania Toshio Nagase amesema amekabidhi tuzo hiyo kwa niaba ya Rais wa Shirika hilo na tuzo hiyo ni ya 14 ambayo hutolewa na Rais wa shirika hilo kwa pamoja na tuzo wanazo toa kwa watu binafsi na mashirika.

Ameongeza kuwa Mhandisi Iyombe ni miongoni mwa watu na mashirika 49 waliopatiwa tuzo za shirika hilo lengo ikiwa ni kuwatambua watu binafsi au Taasisi zinatoa mchango wa kipekee na kugusa maisha ya watu katika kuboresha miundombinu, kuendeleza rasilimali watu, kuboresha maisha ya watu pamoja na kupunguza umasikini katika nchi zinazoendelea.

“Mhandishi Iyombe amefanya yote yanayostahili kupata Tuzo hii tangu wakati akiwa anahudumia Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kisha kuhudumu katika Wizara ya Ujenzi na ndipo kuja hapa OR-TAMISEMI na kote huko alikopita ametoa mchango mkubwa sana katika kuleta maendeleo kwa mtanzania na Taifa kwa ujumla” alisema Nagase.

Aliongeza kuwa mchango wa Iyombe ulianza kuonekana tangu mwaka 1984 mara tu alipomaliza shahada yake ya kwanza ya Uhandisi huko India na kufanya mafunzo kwa vitendo chini ya wataalamu wa Japan waliokua wanajenga barabara ya Kibiti – Lindi.

Kwa kipindi chote cha miaka 34 amejitoka kwa moyo kutumia taaluma yake ya Uhandisi kushiriki kuhudumu ndani na nje ya Tanzania katika miradi mbalimbali ya maendeleo inayosimamiwa na wataalamu kutoka Japan.



Aliyekua Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mhandisi Musa Iyombe (Tatu kulia) akipokea Tuzo ya Utumishi uliotukuta toka kwa Mwakilishi Mkuu wa JICA Tanzania Toshio Nagase

Akizungumza katika hafla hiyo Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mhe. Selemani Jafo amewataka watumishi kufuata nyendo za Mhandisi Iyombe kwa kuwatumikia wananchi kwa moyo ili waweze kuacha alama ‘Legacy’ katika Utumishi wa Umma.

“Tuzo hii anayokabidhiwa Katibu Mkuu wetu asingeweza kupata kama asingekuwa mahiri katika utendaji kazi wake na kujitoka kwa dhati kutatua kero za wananchi; Hii imepelekea yeye kuonekana kati ya wengi kuwa anastahili kutambulika kimataifa, Tuzo hii iwe somo kwetu tuweze kujifunza na kubadilika” alisema Jafo.

“Ni vigumu sana binadamu kumsifia au kuona mazuri ya

binadamu mwenzake kama yuko hai lakini Mhandisi Iyombe una sifiwa ukiwa hai hii inaonyesha kuwa wewe ni kiongozi wa kuingwa kwani ni vigumu kutambua mazuri ya mtu akiwa hai” Alisema Jafo.

Naye Mhandisi Mussa Iyombe amesema kuwa tuzo hiyo sio yake bali ni tuzo ya watumishi wote kwani ushirikiano wao ndo umemfanya akapata tuzo hii kutoka JICA.

“Siwezi sema tuzo hii ni yangu bali tuzo hii ni yetu sote, nasema hivi kwani hapo nilipo bila ushirikiano wenu mimi ni singeweza kupata tuzo hii, kikubwa namshukuru Mungu na tuendeleo kumuomba Mungu ili tudumishe ushirikiano wetu katika utekelezaji wa wajibu tulio nao kwa wataanzania” Alisema Iyombe.



'WAITARA KARIBU TAMISEMI TUCHAPE KAZI' JAFO

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mhe. Selemani Jafo amemkaribisha Mhe. Waitara Mikwabe Mwita (Mb) ambaye amepishwa Nov 2018 kuwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI kujiunga na Timu ya Wizara katika kufanikisha shughuli za maendeleo ya wananchi.

Akimkaribisha kuzungumza na watumishi katika Ofisi ndogo ya Dar es salaam Waziri Jafo amemwambia Mhe. Waitara kuwa Watumishi wa TAMISEMI wanaushirikiano wa hali ya juu na wataaminiwa kufanikisha majuku yako.

“Karibu tuchape kazi hapa kwetu ni kazi tu; Sina shaka na wewe kwakuwa ni rafiki yangu wa siku nyingi na jirani jimboni kwangu hivyo nafahamu fika utendaji wako karibu tuwatumikie wataanzania” alisema Jafo.

Wakati huo huo Waziri Jafo aliwapongeza watumishi kwa weledi waliouonyesha kwa kipindi chote cha uongozi wa Naibu Waziri Mhe. Joseph George Kakunda katika Wizara hii mpaka alipoteuliwa na kuapishwa rasmi kuwa Waziri wa Viwanda Biashara na Uwekezaji.

“Tumepata faraja kubwa sana kwa Mhe. Kakunda kuchaguliwa kuwa Waziri kamili na mafanikio haya ni yetu sote kwani tumefanya naye kazi nzuri zilizopelekea kuteuliwa katika nafasi ya juu zaidi ninawapongeza watumishi wote wa TAMISEMI na ninawasili muendeleze kazi hii nzuri kwa Naibu Waziri Waitara” alisema Jafo.

Naye Naibu Waziri OR-TAMISEMI Mhe. Waitara M. Mwita amesema



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI Mhe. Selemani Jafo (aliyekaa) akimsikiliza Naibu Waziri TAMISEMI Mhe. Waitara Mwita wakati alipowasili kwenye Ofisi Ndogo za Wizara Magogoni Dar es salaam baada ya kuapishwa.

kuja TamiseMI kuboresha shughuli mbalimbali za Wizara na sio kuvuruga hivyo anahitaji ushirikiano wa watumishi waliopo.

“Mimi ni mtu wa kazi na TAMISEMI ninaifahamu kwa sababu nimewahi kuwa mwenyekiti wa mtaa mwaka 2014 na mjumbe wa Kamati ya bunge ya TAMISEMI hivyo ninaifahamu vilivyo Wizara hii; Nataka kutumia uwezo wangu kuboresha zaidi shughuli za Wizara ili tuweze kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi” alisema Waitara.

Aliongeza kuwa tutasumbuana kwenye kazi tu na sio kwenye mambo madogo madogo cha muhimu kwetu sisi ni kazi mengineyo hayana nafasi kwa wakati huu.

Katika uteuzi uliofanyika Novemba 10, 2018 aliyekuwa Naibu Waziri TAMISEMI Mhe. Joseph George Kakunda aliteuliwa kuwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji na nafasi yake kujazwa na Mhe. Waitara Mikwabe Mwita.

Jarida hili hutolewa na:

*Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
S.L.P 1923, Dodoma-Tanzania, Simu: (+255) 26 -2321234*

Barua pepe: ps@tamiseMI.go.tz

Tovuti; www.tamiseMI.go.tz

SERA YA UGATUAJI WA MADARAKA YALETA MABADILIKO

Aliyekuwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mhandisi Mussa Iyombe amasema kuwa Sera ya Ugatuuji wa madaraka imeongeza uelewa na ushiriki wa wananchi katika shughuli za maendeleo.

Iyombe ameyasema hayo wakati akitoa maelezo katika kikao cha mafunzo kwa kamati za kudu-mu za Bunge za Hesabu za Serikali za Mitaa, Utawala na Serikali za Mitaa pamoja na Kamati ya hesabu za Mashirika ya umma kilichoafanyika katika ukumbi wa Bunge, Jijini Dodoma.

Amesema kuwa karibu asilimia 90 ya vijiji na kata zinaandaa na kuwasilisha mipango shiriki-shi kwa wakati na kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa Mipango kwa kutumia mfumo wa fursa za vikwazo katika ujenzi wa shule, vyumba vya madarasa, Ujenzi wa Zahanati, Vituo vya afya na miradi mingine ya maendeleo.

Mhandisi Iyombe amesema kuwa mpaka sasa Serikali ina shule za sekondari za kata zipatazo 3,516 ambazo kwa sehemu kubwa zimejengwa kwa nguvu za wananchi ambapo nguvu hizi zimekuwa zikienda kasi wakati mwingine kutoendana na uwezo wa Serikali wa kuajiri wataalam, vifaa na na fedha za kukamilisha miradi yote iliyoanzishwa na wananchi.

Anafafanua zaidi kuwa Serikali imeweza kuongeza mapato ya ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kutokana na kuongezeka kwa vyanzo vya mapato, uwekezaji na kuimarika kwa mifumo ya ukusanyaji wa mapato na matumizi. Pia mamlaka za Serikali za Mitaa zimeweza kupanga na kupitisha bajeti na kuu-bua vyanzo vya mapato.

Iyombe amesema kuwa dhana ya Ugatuuji wa madaraka kwa Umma inahusu kupeleka madaraka ya kisiasa kwa wananchi lengo likiwa ni kuwapa wananchi madaraka kupitia kwa viongozi wao kuwa na uwezo wa kuamu, kupanga, kutekeleza na kutathmini mipango ya maendeleo kupitia wawakilishi wao, viongozi wa Serikali za Mitaa kuanzia ngazi ya Kijiji na baraza la madiwani la Halmashauri.

Na aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa anayeshughulikia afya Dokta Zainabu Chaula amesema Serikali ime-weza kuboresha

huduma za afya ambapo kwa mwaka 2007 idadi ya vituo vya afya ilikuwa 380 na kata zilikuwa 2500 lakini mwaka 2017/2018 idadi ya kata ni 4,420 na vituo vya afya vimeongezeka hadi kufikia 535.

Amesema Serikali imejikita katika ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya vituo vya afya nchini, kuajiri wataalam wa afya, uboreshaji wa takwimu kwa kutumia mfumo wa kielektroniki (GoTHOMIS), ukokotoaji wa mahitaji halisi ya dawa kwa mfumo mpya na kudhibiti makusanyo ya mapato katika vituo vya huduma pamoja na kuhimiza malipo ya kadi.



Aliyekuwa Katibu Mkuu OR-TAMISEMI Eng. Musa Iyombe akitoa maelezo katika kikao cha mafunzo kwa kamati za kudu-mu za Bunge (hawapo pichani)

Wakati huohuo Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa anayeshughulikia elimu Tixon Nzunda amesema ugatuuji katika elimu hususani Elimu ya Msingi na baadae Elimu ya Sekondari ulitokana na Tamko la Rais la tarehe 12/02/2008 kuhusu kugatua Usimamizi na Uendeshaji wa Shule za Msingi na Sekondari kutoka iliyokuwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwen-da kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa (MSM).

Aidha amesema ugatuuji wa elimu umewezesha kurahisisha Ongezeko la Wanafunzi wa Elimu za Msingi na Sekondari, Takwimu zinaonekana kuwa idadi ya wanafunzi wa Elimu ya Awali imeongezeka kutoka 851,084 (2009) hadi 1,436,322 (2017); Elimu ya Msingi kutoka wanafunzi 8,313,080 (2009) hadi 8,969,110 (2017); Elimu ya Sekondari kutoka wanafunzi 1,293,691 (2009) hadi 1,565,201 (2017).

IDARA YA ELIMU MAWAKILI WA OPRAS

Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Rasilimali watu Idara ya Serikali za Mitaa, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Mohamed Gombati amewataka Maafisa Elimu wa Shule za Msingi na Sekondari wa Halmashauri za Mkoa wa Arusha kuwa mawakili wazuri wa Mfumo wa Wazi wa Tathimini wa Mapitio ya Utendaji Kazi (OPRAS) katika maeneo yao ya kazi ili kuleta utendaji kazi bora katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku.

Gombati ameyasema hayo leo katika Ufunguzi wa Mafunzo ya wawezeshaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa Mkoa wa Arusha ya Mwongozo wa Uboreshaji Matumizi ya Mfumo wa OPRAS kwa Walimu leo Jijini Dodoma.

“Ni imani yangu kuwa baada ya mafunzo haya mtakwenda kuwa wawakilishi makini na mabalozi wa kufanikisha azma ya Serikali ya Awamu ya Tano, yenye kauli mbiu ya “HAPA KAZI TU”, na ikimaanisha kazi hii ni sehemu muhimu katika usimamizi wa utendaji kazi wa watumishi wa umma” Amesema Gombati.

Aidha Gombati ameongeza kuwa mafunzo haya yanawapa jukumu la kwenenda kuwajengea uwezo wakufunzi kwenye ngazi ya Halmashauri (Walimu Wakuu wa Shule za Msingi na Sekondari na Maafisa Elimu Kata) ambao watafanya kazi ya kuwaelekeza walimu katika shule zao na umakini utakao zingatwa hapa utasaidia sana kuhakikisha ufanisi wa azma hii unafanikiwa kwenye ngazi hizo.

Kwa kuhitimisha natambua kuwa mafunzo haya yataleta chachu ya utendaji



Mkurugenzi Msaidizi, Rasilimali watu Idara ya Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Mohamed Gombati akizungumza na maafisa elimu mkoa wa Arusha wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya wawezeshaji wa OPRAS



Picha ya pamoja ni Mkurugenzi Msaidizi, Rasilimali watu Idara ya Serikali za Mitaa, Mohamed Gombati (katikati aliyekaa) pamoja na maafisa elimu mkoa wa Arusha baada ya ufunguzi wa mafunzo

kazi bora wenu kwani mtapata kuwa mnajitathimini kwa kazi mnazo fanya kutokana na malengo mliyojiwekea kwamba baada ya muda flani uweumefikia malengo flani na kwa kutumia mfumo huu basi mnaweza kuendana na kasi ya serikali ya Awamu ya tano, Amesema Gombati.

Naye Afisa Elimu Sekondari Arusha Jiji, Valentine A. Makuka amesema kuwa mafunzo hayo yatawasaidia sana katika kuongeza utendaji kazi bora kwani mfumo huu unamfanya mtu mwenyewe kujitathimini kabla haja tathiminiwa na mkuu wake anaye muongoza.

Ikumbukwe kuwa Mafunzo haya yanaratibiwa na wadau wa maendeleo Uimarishaji Mifumo ya Sekta ya Umma (PS3) kupitia Shirika la USAID.

WALIMU WA SEKONDARI

Hivi karibuni Serikali imetoa waraka wa kuhamisha Walimu wanaofundisha Shule za Sekondari kwenenda kufundisha Shule za Msingi jambo ambalo limeleta sintofahamu kwa jamii hususani Walimu. Akitoa ufafanuzi wa suala hilo Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa anayeshughulikia masuala ya Elimu Tixon Nzunda anasema yafuatayo katika mahojiano maalumu na mwandishi wa makala hii:

Ni vigezo gani vilitumika katika kuhamisha Walimu kutoka Shule za Sekondari kufundisha Shule za Msingi?

Serikali ilifanya tathmini ya kina ili kubaini mahitaji halisi ya Walimu katika kila somo kwa kila shule ya Msingi na Sekondari ndani ya Tanzania Bara na ilijiridhisha pasipokuwa na shaka kuwa kwenye Shule za Msingi kulikuwa na upungufu wa Walimu 97,193. Kwa Shule za Sekondari kulikuwa na upungufu wa walimu 19,000. Masomo ya Sayansi (Hisabati, Fizikia, Kemia, Baiolojia, Biashara, Ufundi na Kilimo) yalikuwa na upungufu mkubwa wa Walimu.

Tathmini hiyo ilibainisha kuwa katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita kumekuwa na ongezeko la Walimu 23,000 wa masomo ya Sanaa katika Shule za Sekondari. Walimu hawa walikuwa wakifundisha vipindi vinne mpaka sita kwa juma moja. Walimu wengine hawakuwa na kipindi hata kimoja hivyo walibaki kusimamia masomo ya jioni ya Wanafunzi. Kutokana na mazingira hayo rasilimali watu haikutumika ipasavyo.

Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali ilifanya uamuzi wa kuwahamisha



Naibu Katibu Mkuu OR-TAMISEMI anayeshughulikia Elimu Tixon Nzunda aki-zungumzia masuala mbalimbali yanayohusu uhamisho wa walimu

Walimu kutoka Shule za Sekondari kwenda Msingi bila kuathiri masharti yao ya kazi. Walimu waliohamishwa kwenda Shule ya Msingi wanabaki na stahili zao za awali. Lengo kuu la Serikali ni kuongeza ufanisi kwa kuimarisha uwiano wa utendaji kazi katika Sekta ya Elimu.

Suala hili halikufanywa na TAMISEMI pekee bali lishirikisha Wizara za Kisekta kama Wizara ya Elimu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, na vyama vya wafanyakazi hasa Chama cha Walimu Tanzania ili kujenga uelewa wa pamoja.

Je, Walimu wanaohamishwa ni wale wenye Shahada au Stashahada au ni wale waliokaa muda mrefu kwenye kituo kimoja cha kazi?

Kigezo cha kwanza cha uhamisho huzingatia sehemu zilizo na idadi kubwa ya Walimu wenye Astashahada (Diploma). Walimu wa Diploma kufundisha shule za msingi hakuna maajabu yoyote. Serikali inalengo la kuimarisha elimu ya msingi na kuwa nguzo ya kukuza elimu na kupunguza pengo la walimu wa shule za msingi na kuwa na uwiano mzuri. Serikali inafanya utaratibu wa kuwatumia walimu.

Serikali inafanya utaratibu wa kuwatumia walimu wenye shahada (degree) kufundisha Shule za Msingi nchini ili kuimarisha ubora wa elimu nchini na vyo vya ualimu vitafanya kazi ya kuimarisha methodolojia shirikishi katika ufundishaji badala ya mfumo uliokuwa umezoeleka lengo ni kuweza kutoa elimu bora kwa watoto wetu.

Waraka ulielekeza kuwa walimu watakaohamishwa wapelekwe kwenye

KUFUNDISHA SHULE ZA MSINGI SIO ADHABU 'NZUNDA'

maeneo ya karibu lakini baadhi ya Walimu waliohamishwa wamekuwa wakilalamika kuwa wamehamishiwa mbali na vituo vyao vya kazi vya awali.

Je, Walimu waliohamishiwa mbali watalipwa stahili zao za uhamisho?

Ili kupunguza gharama za uhamisho wa Walimu, Serikali iliweka kipaumbele cha kuhamisha Walimu walio jirani na Shule za Msingi. Itakapolazimika kumhamisha Mwalimu mbali na kituo cha kazi cha awali. Mwalimu anayehamishwa atastahili kulipwa stahili zake zote za uhamisho.

Serikali imeshatoa maelekezo kwa Maafisa Elimu wote wa Mikoa, Maafisa Elimu wa Wilaya wa Shule za Sekondari na Msingi kuwa Walimu wanaohamishwa mbali na vituo vyao vya kazi vya awali walipwe stahili zao zote.

Fedha za Motisha katika Mpango wa Elimu kwa Matokeo (Education Performance for result - EP4R) zitumike kupitia stahili za Walimu wanaohamishwa. Fedha za EP4R zimeshapelekwa Halmashauri. Aidha kama fedha za EP4R hazitatosha Halmashauri zilipe kupitia vyanzo vya ndani vya mapato.

Baadhi ya Walimu wamekuwa wakilalamika kuwa Maafisa Elimu wamekuwa wakiwahamisha kwenda Shule za Msingi zilizo maeneo ya mbali na kuacha kuwapeleka katika Shule zilizo karibu ambazo zina upungufu wa Walimu. Je, suala hili haliwezi kuwa sababu ya kuwakatisha tamaa Walimu?

Maafisa Elimu wanaohamisha Walimu kwenda shule za mbali na kuacha shule za karibu bila sababu maalum, Serikali haitasita kuwachukulia hatua kali za kinidhamu.

Lengo la kuhamisha Walimu kutoka Shule za Sekondari kwenda Msingi ni kuimarisha uwiano kati ya Mwalimu na Wanafunzi.

Je, Walimu wanaohamishwa kufundisha Shule za Msingi hupewa mafunzo maalum kabla ya kuanza kazi ili kutekeleza majukumu yao mapya?

Ufundishaji wa Wanafunzi wa Sekondari na Msingi hautofautiani sana kwa sababu elimu zote huzingatia saikolojia ya watoto. Hata hivyo, Serikali inakusanya fedha ili kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo Walimu hao.

Je, ni sababu zipi husababisha Walimu kutopewa vibali vya uhamisho pindi wanapotaka kuhama vituo kwa ridhaa yao wenyewe?

Ili kudhibiti upungufu wa Walimu katika maeneo ya Vijijini, Serikali huzuia Utumishi wanaopenda kuhamia maeneo ya mijini na kuacha mapengo katika vituo vyao vya kazi bila sababu ya msingi. Serikali itaruhusu Mwalimu au mtumishi yeyote kuhama pale ambapo kutakuwa na sababu za kimsingi kama vile upungufu wa walimu, afya au usalama wa mtumishi pamoja na sababu nyingine zinazokubalika katika Utumishi wa Umma.

Utaratibu wa kuhamisha Walimu kutoka Mkoa mmoja kwenda mwingine hufanywa na Ofisi ya Rais TAMISEMI. Kutokana na idadi ya maombi ya uhamisho wa Walimu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kufikia 13,000, Ofisi imeunda Timu itakayofanya upembuzi utakaozingatia hali halisi ya mazingira. Taarifa ya jumla ikikamilika itatolewa kupitia tovuti OR – TAMISEMI.

Wito wangu kwa Walimu waliohamishwa kutoka shule za Sekondari na kwenda shule za msingi kuhakikisha wanaripoti katika vituo walivyopangiwa na kufundisha kwa moyo, Serikali itatoa ushirikiano pale panapohitajika.

Dondoo Muhimu

DIRA YA OR-TAMISEMI

Kuwa Taasisi inayoongoza katika kuziwezesha Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kutoa huduma bora zaidi kwa jamii ili kuboresha hali zao za maisha na kuondokana na umaskini.

WATAALAMU WA MIPANGO WAPIGWA MSASA, MAANDALIZI YA BAJETI 2019/20

Aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia masuala ya Afya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Dk. Zainabu Chaula amewataka Makatibu Tawala Wasaidizi wa Mikoa Sehemu ya Mipango na Uratibu sambamba na Maafisa Mipango wote wa Halmashauri nchini kutumia taaluma zao katika kukuza uchumi wa nchi ili kuleta matokeo chanya kwa jamii.

Dk. Chaula ameyasema hayo wakati wa Ufunguzi wa Mafunzo ya Maandalizi ya Mipango na Bajeti katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa Fedha 2019/20 yanayofanyika kwa siku mbili Jijini Dodoma katika ukumbi wa Mikutano wa Royal Vilage Hotel.

Dk. Chaula amesema mafunzo hayo ni fursa kwa maafisa hao kuhakikisha wanapata ujuzi na uelewa zaidi wa namna sahihi ya uandaaji wa Mipango na Bajeti katika Mikoa na Halmashauri.

“Ili kufikia matokeo bora ya kukuza uchumi wa nchi hii mnatakiwa kuwa wabunifu na kuhakikisha mnabadilisha changamoto kuwa fursa kitu ambacho kitabadili dhana iliyopo kwa sasa kwa wananchi kulalamikia changamoto hizo na badala yake wazitumie kuwa fursa za kuwaletea maendeleo” Alisema Dk. Chaula.

Alongeza kuwa sisi wataalamu tupo hapa kwa niaba ya wananchi hivyo tunatakiwa kuleta mipango itakayoweza sha wananchi hao kujikwamua kiuchumi na kujiletea maendeleo endelevu na hili litafikiwa endepo mipango na bajeti inakwenda sambamba na fursa zinazopatikana katika maeneo yetu

Aidha Dk. Chaula ameongeza kuwa kila mtumishi wa Umma anadhamana kubwa kwa taifa na dhamana yenyewe ni kuhakikisha tunawatumikia vyema watanania wenzetu ili kuleta matokeo bora kwa nchi yetu kama Muhasisi wa Taifa hili Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alivyo fanya na mpaka leo kupitia matokeo yake tunamkumbuka.

Aidha Mkurugenzi wa Idara ya Sera na Mipango OR-TAMISEMI Bw. John Cheyo, amesema kuwa kupitia mafunzo hayo maafisa hao watapata uelewa aidi ya namna ya kuandaa bajeti iliyobora na halisi na zaidi watakuwa waliimu wazuri kwa maafisa wengine katika maeneo yao ya kazi ambao hawajabahatika kupata mafunzo haya.

Naye Mkurugenzi wa Mradi wa Uimarishaji Mifumo ya Sekta ya Umma (PS3), Dk. Emanuel Malangalila amewataka kuwa maafisa waliopata mafunzo haya wakatumie wakatumie elimu hiyo kuleta matokeo bora katika maeneo yao ya kazi ikiwemo kukuza uchumi na kupunguza umasikini katika mikoa na halmashauri zao.

Akihitimisha kwa neno la shukurani kwa niaba ya washiriki wenzake Katibu Tawala Msaidizi Mipango na Uratibu kutoka Ruvuma Edmundi Godwell Siame amesema yote yaliyoelekezwa kupitia ufunuzi wa mafunzo hayo sambamba na elimu watakuoipata watazingatia na kufanyia kazi ili kuhakikisha taaluma yao inakuwa nyenzo muhimu katika kukuza uchumi wa Nchi.



Naibu Katibu Mkuu OR-TAMISEMI anayeshughulikia Afya Dkt. Zainabu Chaula akifungua kikao cha Makatibu Tawala Wasaidizi Sehemu ya Mipango na Uratibu



Makatibu Tawala Wasaidizi Sehemu ya Mipango na Uratibu wakiwa kwenye mafunzo ya maandalizi ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2019/20

UKARABATI WA SHULE KONGWE MOTISHA KWA WANAFUNZI

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mhe. Seleman Jafo hivi karibuni alifanya ziara katika baadhi ya shule kongwe zilizofanyiwa ukarabati kukagua maendeleo ya ujenzi na kuzungumza na wanafunzi pamoja na walimu.

Akizungumza katika shule ya Sekondari ya Wasichana ya Ruvu alisema kuwa Serikali ya awamu ya Tano imetenga sh. bilioni 45 kwa ajili ya mpango maalum wa ukarabati mkubwa na uboreshaji wa miundombinu mbalimbali yakiwemo madarasa, mabweni na nyumba za waalimu kwa shule zote kongwe nchini.

Aliongeza kuwa mpango huu umehusisha shule Kongwe 88 katika awamu ya kwanza na inatekelezwa kwa kipindi cha miaka miwili. Mpaka sasa shule 44 kati ya 89 ziko kwenye hatua mbalimbali za ukarabati.

Alisema kuwa shule nyingi zimejengwa kipindi cha ukoloni kutokana na kutofanyiwa ukarabati wa mara kwa mara majengo yake yamechakaa na hayavutii kabisa.

“Mazingira yaliyokuwepo hayamvutii wala kumhamasisha mwanafunzi kusoma kwa bidii na kwa kuliona hilo Serikali imechukua hatua stahiki kwa kuboresha mazingira ya kufundisha na kujifunzia” alisema Jafo.

Aliongeza kuwa ili kuboresha kiwango cha elimu na kurudisha hadhi ya shule Kongwe na kuongeza ufaulu tumeona mazingira bora yanaweza kuljibu maswali yote hayo ya Tanzania.

Akifafanua kuhusu mpango huu Naibu Katibu Mkuu Elimu Tixon Nzunda



Muonekano wa juu wa shule ya sekondari Pugu baada ya kufanyiwa ukarabati ikiwa ni miongoni wa shule kongwe zilizoko kwenye mapango wa ukarabati

amesema vipaumbele vya Serikali katika sekta ya Elimu ni uboreshaji wa miundombinu yote katika shule pamoja na makazi ya walimu.

Nzunda aliongeza kuwa kwa sasa awamu ya kwanza ya ukarabati wa shule hizo 45 umefikia katika hatua nzuri na unaendelea mpaka shule zote 89 zitakaapokamilika.

Aliongeza kuwa Serikali imendelea kukarabati shule nyingine za kata na shule za msingi na zoezi hilo linafanyika kupitia fedha za lipa kutokana na matokeo (EP4R).

Aidha Nzunda amewaomba wadau wa Elimu kuendelea kushirikiana na Serikali kusaidia kujenga miundombinu ili kuzidi kuboresha mazingira ya upatikanji wa Elimu Nchini.

Naye Zakia Abdala mwanafunzi wa Kidato cha Tano Ruvu Sekondari alisema kuwa ukarabati wa shule yao ni motisha kwao kuzidi kujisomea na kufanya vizuri kwenye mitihani yao.

“Ujue hapo awali ulikua huwezi kutamani kurudi shuleni baada ya muda wa likizo kwa sababu ya uchakavu wa miundombinu kuanzia darasanu, bwenini mpaka vyooni hali ilikua mbaya sana lakini baada ya ukarabati huu tunashinda darasani kusoma na ukirudi bwenini unapumzika vizuri hii itatusaidia sisi kuzingatia masomo yetu na kuachana na mawazo ya kufikiria nyumbani na tunamuahidi Waziri wetu kuwa tutafauku vizui mitihani yetu “ alisema Zakia.

ASTASHAHADA, STASHAHADA MSIZIPE KISOGO: WAZIRI JAFO



Waziri wa Nchi OR-TAMISEMI Mhe. Selemani Jafo (katikati aliyekaa) katika picha ya pamoja na viongozi wa chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo baada ya uzinduzi wa bustani ya Mgufuli iliyopo chuoni hapo

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mhe. Selemani Jafo amesema kuanza kwa kozi za ngazi ya Shahada katika Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo kisiwe kigezo cha kuondosha kozi za Astashahada na Stashahada katika chuo hicho.

Waziri Jafo alikuwa akizundua rasmi Bustani ya Magufuli katika chuo hicho ambapo Bustani hiyo itatumika kuishi na kuenzi mchango wa kiongozi huyo wa Nchi kwasasa ambao ni uzalendo, kujituma pamoja na uadilifu katika kuwatumikia wananchi.

“Nimesikia maombi yenu yakutaka Kuanzishwa kwa kozi za Ngazi ya Shahada kusudi mtu anapo hitimu masomo yake ya ngazi za awali aweze kuendelea, namo niwambie, tutajitahidi lifanikiwe, lakini angalizo langu kwenu, tutakapo anzisha Degree isiwe sababu yakusitisha kozi zinazoendelea kwa sasa, ikiwepo Astashahada (Certificate) na Stashahada (Diploma) ya kozi mnazo endelea nazo” amesema Jafo.

Waziri Jafo amesema, vyuo vingi vilipo anzisha ngazi ya Shahada na kusahau wataalam wa kada za kati vilichochea kukosekana kwa wataalam wakutosha katika ngazi ya kati hususan mafundi mchundo ambao walikuwa wakizalishwa katika vyuo hivyo.

Katika hatua nyingine Waziri Jafo amewahakikishia Wakurufunzi hao wa chuo cha Hombolo uhakika wa kuajiriwa na Serikali kwa wale watakapo fikia vigezo vinavyo hitajika katika nafasi mbali mbali ambazo serikali itatangaza.

“Tumebaini Wataalam wa chuo cha Hombolo tunaowaajiri katika kada za Maafisa Watendaji wa Vijiji, Kata na hata Tarafa wanauelewa mpana wa Masuala ya jamii za watanzania hususan ni wale waishio vijijini, hivyo basi tunapotangaza ajira kipaumbele tutakitoa kwa wanafunzi wa chuo hiki” amesema Waziri Jafo.

Mhe. Jafo hakusita kuonesha furaha yake kwa jinsi chuo hicho kilivyo jizatiti katika suala la utunzaji wa mazingira, hatua ambayo ameitaja ni kumuunga mkono Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan ambaye kupitia Wizara ya Mazingira na Muungano amekuwa mstari wa mbele kuhakikisha watanzania wanantunza mazingira.

Mbali ya pongezi hizo Waziri ametoa maelekezo kwa uongozi wa Manispaa ya Dodoma kuanza kampeni ya upandaji wa miti ya Matunda. “Tunataka Dodoma iwe Fruit City” amenukuliwa Waziri

Inaendelea Uk17

KAMATI YA BUNGE YA UGANDA YAMWAGIA SIFA MRADI WA DMDP

Kamati ya bunge ya hesabu za Serikali za Mitaa kutoka Nchini Uganda (PAC-LG) imemwagia sifa Mradi wa Uendelezaji wa Jiji la Dar es salaam unaoendelea kutekelezwa katika Manispaa ya Tano za Mkoa wa Dar es salaam.

Kamati hiyo yenye zaidi ya wajumbe kumi waliotemebelea Mradi wa **DMDP** unaotekelezwa chini ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa wamesema ni mradi wa mfano na kuigwa na Nchi za Afrika Mashariki zinazopata mkopo wa fedha kutoka Benki ya Dunia.

Akizungumza katika ziara hiyo ya mafunzo Mwenyekiti wa Kamati hiyo (PAC-LG) Mhe. Ronald Reagan Okumu amesema lengo la ziara yao ni kuona namna ambavyo miradi ya Uboreshaji Miundombinu inayotekelezwa kwa fedha za Mkopo toka Benki ya Dunia;

“Tunapenda kuona ubora wa miradi hiyo, taratibu za ulipaji fidia zilivyofuata, maelekezo ya mkopo wa fedha hizo yalivyozingatiwa na zaidi namna ambavyo fedha zilivyopokelewa, zinavyosimamiwa na wataalamu, zinavyotumika na zinafanyiwa ukaguzi na zaidi suala zima la thamani ya fedha” **Value for Money**” kuonekana katika miradi hiyo” alisema Mhe. Okumu.

Akipokea ujumbe huo toka Bunge la Uganda Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa **Mhe. Josephat Kandege** amesema mradi huu ume-tekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu sasa na mafanikio yaliyopatikana ni makubwa na kwa kiasi kikubwa umesaidia kuwapunguzia kero wananchi wa Mkoa wa Dar es salaam.

“Karibu mjifunze kwa kuona mtaona barabara zilivyojengwa kwa ubora wa hali ya juu, njia za bora waenda kwa miguu, mifereji yenye viwango ya kusafirishia maji ya mvua, masoko na ofisi za miradi pamoja na maabara za kisasa za kupima ubora wa barabara zinazoendelea kujengwa” alisema Kandege.

Akielezea Miradi inayotekelezwa chini ya fedha za Mkopo wa Benki ya Dunia Mratibu wa Miradi hiyo toka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Eng. Davis Shemangale amesema kuwa mradi huu unatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano na una lengo la kuboresha Jiji la Dar es Salaam lizidi kuwa bora katika Sekta ya miundombinu, usafiri mjini pamoja na usalama

Eng. Shemangale aliongeza kuwa mradi huo pia uta-boresha makazi bora sambamba na kujenga uwezo wa

Kitaasisi pamoja na mifumo stahiki na ya kutosha kutunza kumbukumbu na takwimu itakayosaidia katika Ukusanyaji wa mapato.

Naye mratibu wa mradi wa uendelezaji wa Jiji la Dar es salaam (DMDP) **Eng. Emmanuel Ndyamukama** amesema Katika awamu ya kwanza ya mradi huu itagharimu jumla ya Dola za Kimarekani Milioni 300 ambazo ni Fedha za Mkopo kutoka Benki ya Dunia. Aidha Shirika la maendeleo la Nchi za Nordic litatoa ruzuku ya dola za kimarekani Mil. Tano kwa ajili ya kukabili changamoto za mabadiliko ya Tabia ya Nchi na huku Serikali ya Tanzania ikichangia takribani Dola za Kimarekani Mil. 25.3 kwa ajili ya kulipa fidia wananchi walioathirika na mradi.

Kamati ya Bunge ya hesabu za Serikali za Mitaa iko katika ziara ya mafunzo kwa muda wa siku Tano na itatemebelea miradi ya uendelezaji wa Jiji la Dar es salaam (DMDP), Mabasi yaendayo haraka (BRT) kasha kuelekea katika Manispaa ya Morogoro ambako wataemebelea mradi wa uboreshaji na uimarishaji wa Mamlaka za Miji (ULGSP) kasha kumalizia na Jiji la Dodoma ambako watajione mradi wa Uboreshaji Miji Kimkakati (TSCP).



Naibu Waziri OR-TAMISEMI Mhe. Josephat Kandege akipokea ujumbe wa kamati ya bunge ya hesabu za Serikali za Mitaa toka Nchini Uganda

Inatoka Uk2

inabidi tuongeze usimamizi katika maeneo yetu. Tunafanya vizuri lakini kuna kazi ya kufanya maa-na watu bado wana mioyo ya kishetani."

Jafo aliwataka wakuu hao kuhakisha ripoti za wakaguzi wa ndani zinajadiliwa vizuri ili mambo ambayo hayajakwenda vizuri yajadiliwe mapema na kuchukua hatua kwa haraka.



Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Mhe. John Mongela akitoa neno la shukrani kwa niaba ya Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala walioshiriki kwenye Mafunzo ya Uongozi



Waziri wa Nchi OR-TAMISEMI Mhe. Selemani Jafo (katikati mbele) katika picha ya pamoja na viongozi wa Tamisemi, Taasisi ya Uongozi na baadhi ya Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala Mikoa baada ya kupokea vyeti vyao vya ushiriki wa mafunzo



Waziri wa Nchi OR-TAMISEMI Mhe. Selemani Jafo (kulia) akimkabidhi Mkuu wa Mkoa wa Kagera Brigedia Jenerali Marco Gaguti cheti baada ya kushiriki kikamilifu kwenye mafunzo ya Uongozi

Aidha, Jafo aliagiza viongozi hao kuhakikisha kuwa, hospitali za wilaya zinaanza kujengwa na kuwataka kuhakikisha wanamaliza mivutano iliyoibuka ya wapi hospitali hizo zijengwe ambayo pia imechangiwa na siasa na inapoteza muda wa kuanza ujenzi huo.

Pia Jafo amewaagizi viongozi hao kusimamia kwa kарибу utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwemo ile ya afya, barabara na kusisitiza kusimamaia nidhamu na uwajibikaji kwa watumishi sambamba na utoaji asilimia 10 ya fedha za mapato ya ndani kwa ajili ya wanawake, vijana na wenye ulemavu kama sheria inavyobainisha.

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Uongozi, Profesa Joseph Sembojaalisema ratiba ya mafunzo ya wiki moja ilibana kwasababu ya mambo mengi waliyopitia.

Alisema mafunzo hayo wamejenga uwezo wa viongozi na kwamba kuna maeneo matatu ambayo angependa wawe na yao kama viongozi.

Aliyataja maeneo hayo ni kuwa Kiongozi wa kimkakati, kuhakikisha rasilimali watu na nyingine kuhakikisha kuwa zinatumiwa ipasavyo pamoja na kuwa kiongozi wa kuigwa kwa kuwa na sifa za kimaadili.

BIL 77 ZA TSCP ZATEKELEZA AGIZO RAIS JPM

JIJINI DODOMA

Mradi wa Mpango Miji Mkakati 'Tanzania Strategic Cities Project' maarufu kama **Tscp** unaosimamiwa na Ofisi ya Rais TAMISEMI umetekeleza Agizo la Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kutoa Fedha zaidi ya Tsh. Bil 77 kwa ajili ya kujenga miundombinu katika Jiji la Dodoma.

Akizungumza katika hafla ya utiaji saine miradi hiyo itakayotekelezwa kupitia mradi wa **Tscp** Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TamiseMI **Mhe. Selemani Jafo** amesema mradi huu wa kimkakati umelenga kubadilisha kabisa muonekano wa Jiji la Dodoma kwa kutekeleza yale aliyoagiza Mhe. Rais alipotangaza kuipandisha hadhi iliyokuwa Manispaa ya Dodoma kuwa Jiji.

"Jiji hili lazima liwe la tofauti, lenye hadhi ya Makao Makuu ya Nchi na livutie kuliko majiji yote Tanzania, tutaweka miundombinu ambayo itabadilisha kabisa muonekano wa Jiji, itaongeza fursa za biashara na kuwapunguzia kabisa adha wananchi wetu katika maeneo ambayo wamekuwa wakiyalalamikia.

Tunaimani kupitia kazi itakayofanyika hapa mtu aliyeondoka Dodoma mwaka huu akirudi baada ya miaka miwili tutamshika mkono kumuelekeza mitaa ya Jiji la Dodoma, hapatakuwa kama palivyo sasa na mabadiliko yatayofanyika ni ya kimataifa" Alisema Jafo.

Kupitia hafla hiyo Mhe. Jafo aliwatahadharisha wakandarasi washauri wa mradi kusimamia mradi huo kwa mujibu wa taratibu na sheria na kuhakikisha thamani ya fedha inaonekana kwa kila kipengele kitakachotekelezwa.

"Mkandarasi mshauri wajibu wenu ni kuhakikisha kila kilichoainishwa kiinafanyika kwa wakati na kwa usahihi wakati huo huo kumshauri mteja wao ambaye ni Halmashuri kufanya yale yote yanayotakiwa ili kazi iende sawa na kumsimamia mkandarasi kufanya kazi hiyo kwa ubora wa hali ya juu na endapo utaenda kinyume na haya Wizara yangu haitasita kukuchukulia hatua kwa mujibu wa sharia" alisema Jafo.

Inaendelea Uk.....17

Alimazia kuwa Ofisi ya Rais TAMISEMI inatekeleza miradi mikubwa mitatu kwa fedha za mkopo tokaq Benki ya Dunia zenye lengo za kuimarisha na kuboresha Halmashauri za Majiji, Manispaa, Miji pamoja na Mkoa mzima wa Dar es es Salamm ili mamlaka hizo ziweze kukua kulingana mabadiliko tunayokwenda nayo kuelekea uchumi wa kati na ziweze kutoa huduma bora kwa wananchi wake.

Jafo alitaja miradi mikubwa ya miundombinu inayosimamiwa na Ofisi yake kuwa ni Mradi wa Mpango Miji Mkakati (Tscp) unatekelezwa kwenye Majiji na Manispaa 8 na Dodoma ikiwa ndani ya mradi huu ambao utagharimu jumla ya fedha za kitanzania sh Bil 840, Mradi wa Uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam (Dmdp) ambao ni maalumu kwa kushughulikia changamoto za Jiji la Dar es salaam nao utagharimu Tsh. Bil 660 pamoja na Mradi wa Uendelezaji na Uboreshaji wa Halmashauri za Miji (Ulgsp) unatekelezwa katika Miji 18 na unagharimu Tsh. Bil. 650.

Naye Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu ambaye pia ni Mbunge wa Dodoma **Mhe. Antony Mavunde** akizungumza katika hafla ya utiaji saine wa miradi ya miundombinu katika Jiji la Dodoma ameshukuru Serikali kwa kuleta Fedha kwa ajili ya ujenzi wa miradi itakayofungua milango ya maendeleo katika Jiji la Dodoma.

Pia aliwakumbusha wananchi wa Dodoma kuitumia fursa hii ya upatikanaji wa miradi mikubwa kama chachu ya maendeleo ambayo itakuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla na kubadilisha maisha kutoka yalivyo sasa na kuwa bora zaidi.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Dodoma **Mhe. Bilinith Mahenge** amesema miradi hii ni fedha nyingi sana na Serikali imeamua kuwekeza katika Jiji hili hivyo yeye kama msimamizi Mkuu wa shughuli za Mkoa huu atahakikisha atasimamia kwa karibu miradi hii ili ikamilike kwa wakati na kwa ubora wa hali ya juu.



Huu ndio muonekano wa Stendi ya Kisasa itakayojengwa katika Jiji la Dodoma kupitia mradi wa

BIL 2.8 ZALETA NEEMA TARURA

Kutokana na uchanga wa Wakala wa barabara za Vijijini na Mijini(TARURA) ambapo ina mwaka sasa tangu kuanzishwa kwake bado inakabiliwa changamoto ya uhaba wa vitendea kazi, majengo ya Ofisi katika ngazi ya Halmashauri na Mikoa pamoja na ufinyu wa bajeti ikilinganishwa na mahitaji.

Katika kukabiliana na changamoto hizo eneo la uhaba wa vitendea kazi ambalo ni pamoja na magari ya usimamizi wa kazi mbalimbali zinazotekelezwa na TARURA, Serikali kwa kuliona hilo imeona ni vyema kutatua changamoto katika maeneo mbalimbali yenye Uhitaji hususani uhaba wa vitendea kazi kama magari ya usimamizi wa shughuli za barabara.

Lengo ni kuongeza ufanisi katika utendaji kazi na hatimaye kucheza kazi ya ukuaji wa uchumi nchini.

Katika Mwaka wa Fedha 2017/18 Serikali imetumia zaidi ya Tsh Bil. 2.8 katika ununuzi wa magari 26 ambayo yamekabidhiwa kwa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa barabara za vijijini na mijini (TARURA) na kufanya Wakala kuwa na idadi ya magari 288 kati ya Magari 440 yanayohitajika.

Akikabidhi magari hayo Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za **Mitaa Mhe. Selemani Jafo** amesema magari haya yanayokabidhiwa yakasaidie katika kufuatilia utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa Barabara ili kuhakikisha kuwa kila shilingi inayotolewa na Serikali inatumia kwa malengo yaliyokusudiwa.

“Natoa Rai kwa **TARURA** mhakikishe mnayatunza magari haya ili yakafanikishe malengo ya ujenzi na ukarabati wa barabara kwa ufanisi, na madereva wote watakaokabidhiwa wapewe maelekezo ya kuwa makini katika kuyahudumia ipasavyo kila inapotakiwa ili yaweze kuduma kwa muda mrefu” alisema Jafo.

Pia aliwakumbusha wataalamu wote wa **TARURA** kufanya kazi kwa Weledi ili kuleta matokea ya haraka katika sekta ya barabara ambayo inategemewa sana na imekua chachu katika kukuza uchumi wa Taifa letu.

Naye Mtendaji Mkuu wa TARURA Mhandisi Victor Seif ameishukuru Serikali kwa kuwapatia magari ambayo tataongeza ufanisi katika utendaji kazi wa TARURA pia alibainisha kuwa katika Bajeti ya mwaka wa Fedha 2018/19 Serikali imetenga Tsh. Bil 2 kwa ajili ya kununua magari mengine 20.

Serikali ilianzisha Wakala wa Babarabara za vijijini na mjini (TARURA) kwa sharia ya Wakala wa Serikali Sura ya 245 na kutangazwa rasmi kwenye Gazeti la Serikali Na. 211 la tarehe 12/05/2017 na kuzinduliwa rasmi mnamo mwezi Julai, 2017 na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa(MB).



Waziri wa Nchi OR-TAMISEMI Mhe. Selemani Jafo (aliesimama) akizungumza wakati wa hafla ya kukabidhi magari 26 ya TARURA, kushoto kwake ni Mtendaji Mkuu wa TARURA Eng. Victor Seif.



Waziri wa Nchi OR-TAMISEMI Mhe. Selemani Jafo (Katikati) akikata tepe kuashiria uzinduzi wa magari 26 yaliyonunuliwa na Serikali na kuyakabidhi TARURA kwa matumizi katika Halmashauri mbalimbali Nchini.



Baadhi ya magari yaliyokabidhiwa kwa TARURA.

Inatoka Uk.. 15

Akiwasilisha taarifa mradi Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma Godwin Kunambi ametaja kazi zitakazofanyika kupitia mradi wa TSCP kuwa ni Ujenzi wa barabara za Lami Km 26.6, Taa za barabrani 913, mfereji mkubwa wa kusafirishia maji ya mvua Km 6.5, Ujenzi wa Stendi ya Kisasa, Soko kuu la Kisasa, vizimba 7 vya kukusanyia taka, kituo kikuu cha kuegesha malori pamoja na bustani ya kupumzikia yenye viwanja mbalimbali vya michezo.

Aliongeza kuwa barabara za lami zitajengwa maeneo ya katikati ya mji, pembezoni pamoja na barabara moja kubwa ya mchepuko zitajengwa kwa kiwango cha Lami Ngumu (Concret Asphat) na zitakuwa na eneo la waenda kwa miguu, mifereji ya maji ya mvua pamoja na Taa za barabara zinazotumia nguvu ya jua.

Akizungumzia ujenzi wa stendi ya kisasa itakayojengwa eneo la Nzuguni Kunambi amesema itajengwa kwenye eneo lenye ukubwa wa Ekari 87 itakua na uwezo wa kuegesha Mabasi Makubwa 250, Mabasi madogo na magari ndogo 600, Bajaji 300 na pia itakua na maeneo makubwa ya biashara pamoja na eneo maalumu kwa ajili ya wafanyabiashara ndogondogo (Machinga) pamoja na mama lishe.

BODI YA UHARIRI

Mhariri Mkuu: Rebecca Kwandu

Msanifu: Nteghenjwa Hosseah

Waandishi: Angela Msimbira, Fred Kibano, Atley Kuni, Rafael Kilapilo na Nteghenjwa Hosseah.



Waziri wa Nchi OR-TAMISEMI Mhe. Selemani Jafo akizungumza wakati wa utiaji saina mikataba ya ujenzi wa miradi ya TSCP Jijini Dodoma



Viongozi wa Jiji la Dodoma pamoja na wakandarasii wakisaina mikataba ya ujenzi wa miradi ya TSCP Jijini Dodoma



Waziri wa Nchi OR-TAMISEMI Mhe. Selemani Jafo katika picha ya pamoja na viongozi wa Jiji la Dodoma baada ya utiaji saina mikataba ya ujenzi wa miradi ya TSCP Jijini

Inatoka Uk...12

Kwa Upande wake Mwenyekiti wa Bodi inayomaliza Muda wake Prof. Suleiman Ngware, yeye alisema lengo la kujenga Bustani ya Magufuli nikuunga mkono juhudi za Mhe. Rais katika kusimamia rasilimali za nchi kwa moyo uzalendo na uadilifu wa dhati.

"Mhe. Waziri Shabaha yakuwa na Bustani ya aina hii yenye Mnara wa Magufuli nikutambua mchango mkubwa na moyo wa kizalendo alionao Rais wetu, sasa tunachotaka nini hapa, kila mtu atakaye uanalia mnara huu aweze kujitathmini mwenyewe bila yakusukumwa na mtu, Je! Mimi kama Mkufunzi ninatimiza wajibu wangu? Mimi kama Mwanafunzi nafanya matendo sawa na Rais wangu? Mimi kama Mwenyekiti wa Bodi au Mkuu wa Shule sifanyi manyanyaso kwa watu sibagui watu". Amesema Mwenyekiti huyo.

Kila Mwaka ifikapo Aprili 18, Bodi, Uongozi, Wanafunzi na Wananchi wanaozunguka eneo la chuo watakuwa wakikutana kwa pamoja na kujitathmini kwa mienendo na matendo yao ya utendaji wa mwaka mzima, Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo kwa sasa kinawanafunzi zaidi ya 3000

ARUSHA & DODOMA VINARA UKUSANYAJI WA MAPATO

Halmashauri ya Jiji la Dodoma na Arusha zimeibuka vinara katika ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa robo ya kwanza ya mwaka wa Fedha 2018/19.

Hayo yamebainishwa jana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Selemani Jafo alipokuwa akitoa ya mapato ya ndani ya halmashauri kwa robo ya kwanza ya mwaka.

Alisema Halmashauri ya Jiji la Dodoma imeongoza kwa kukusanya mapato ghafi kwa kukusanya Sh bilioni 14.49 kati ya makisiso ya kukusanya Sh bilioni 68.6 ambayo ni sawa na asilimia 21.

Aidha, Arusha inaongoza kwa kukusanya vizuri kiasilimia na imefanikiwa kukusanya Sh bilioni 4.1 kwa asilimia 26 ya malengo waliyojiwekea ya kukusanya Sh bilioni 15.6.

“Teleweke wazi kuwa Jiji la Arusha ndio lililofanya vizuri kimakusanyo kwa mujibu wa asilimia lakini Jiji la Dodoma ndio lililokusanya fedha nyingi zaidi kuliko halmashauri zote Tanzania,” alisema.

Alisema kwa mwaka wa Fedha 2018/19, halmashauri zili-pangiwa kukusanya Sh bilioni 735.6 kutoka kwenye vyanzo vyaake vya ndani na hadi kufikia Septemba 30 mwaka huu Halmashauri zilikusanya jumla ya Sh bilioni 143.6 sawa na asilimia 20 ya makisiso ya mwaka.

Alisema kwa mwaka wa fedha 2017/18 Halmashauri zili-pangiwa kukusanya Sh bilioni 687.3 na hadi kufikia septemba 30 mwaka 2017 ziliweza kukusanya Sh bilioni 126.8 sawa asilimia 18 ya makisiso ya mwaka.

“Kutokana na Takwimu hizo inaonyesha kwamba Halmashauri zimeongeza wingi wa mapato kwa kiasi cha Sh bilioni 16.7 na ufanisi wa ukusanyaji wa mapato ya ndani umeongezeka kwa asilimia 2” alisema Jao.

“Uchambuzi wa mapato ya ndani ya robo mwaka ya mwaka wa fedha 2018/2019, unaonesha kuwa jumla ya halmashauri 76 zimefanya vizuri kwa kukusanya zaidi ya asilimia 20 ya makisiso yake ya mwaka.

Kati ya halmashauri hizo Majiji ni 4, zikiongozwa na halmashauri ya jiji la Arusha, manispaa 7 zikiongozwa na manispaa ya Musoma, miji 12 ikiongozwa na mji wa

Aidha, Halmashauri 23 zimefanya vibaya kwani zimekusanya chini ya asilimia 10 ya makisiso yake ya mwaka. Halmashauri hizo ni pamoja na halmashauri za miji 3 na halmashauri za wilaya 20 ambapo halmashauri ya mwisho kabisa ni halmashauri ya Wilaya ya Masasi ambayo imekusanya sawa na asilimia mbili ya makisiso ya mwaka,”

Akisoma mchanganuo wa ukusanyaji mapato kwa vigezo mbalimbali, Jafo alisema halmashauri 10 zimefanya vizuri zaidi kwa kukusanya mapato kiasilimia ikiongozwa na Kisarawe DC iliyokusanya Sh bilioni 1.2 ambayo ni sawa na asilimia 55.

Halmashauri zingine ni Kilwa DC iliyokusanya Sh bilioni 1.45 (asilimia 43), Tarime DC Sh bilioni 1.8 (asilimia 39), Meatu Sh bilioni 1.2 (asilimia 36), Kite-to Sh milioni 760.49 na Mbinga Sh milioni 511.71 (asilimia 35), Babati DC Sh milioni 952.57 (asilimia 33) Mpwapwa Sh milioni 574.4 (asilimia 33), Kongwa DC Sh milioni 826.79 (asilimia 33) na Hai Sh milioni 413.65 (asilimia 33).

Jafo alitaja halmashauri tatu zilizokusanya mapato mengi (ghafi) bila kujali asilimia ya ukusanyaji kuwa ni Dodoma MC iliyokusanya Sh bilioni 14.49 ambayo sawa na asilimia 21, Ilala MC iliyokusanya sh bilioni 11.2 sawa na asilimia 20 na Kinondoni MC iliyokusanya Sh bilioni 7 sawa na asilimia 21.

Jafo alisema halmashauri 24 zimekusanya mapato ya zaidi ya Sh bilioni moja kuwa ni Dodoma MC (Sh bilioni 14.49), Ilala MC (Sh bilioni 11.21), Kinondoni MC (Sh bilioni 7), Temeke MC (Sh bilioni 6.56), Arusha CC (Sh bilioni 4.1), DSM CC (Sh bilioni 3.96), Mwanza CC (Sh bilioni 3.9), Ubungo MC (Sh bilioni 3.47), Tanga CC (Sh bilioni 2.72).

Pia Tarime DC (Sh bilioni 1.86), Mbeya CC (Sh bilioni 1.69), Ilemela MC (Sh bilioni 1.55), Kahama TC (Sh bilioni 1.53), Geita TC (Sh bilioni 1.45), Kilwa DC (Sh bilioni 1.45), Morogoro MC (Sh bilioni 1.2), Chalinze DC (Sh bilioni 1.36), Kishapu DC (Sh bilioni 1.3), Mkuranga DC (Sh bilioni 1.2), Kigamboni MC (sh bilioni 1.2), Meatu (sh bilioni 1.2), Kisarawe (Sh bilioni 1.2), Moshi MC (Sh bilioni 1.18) na Tunduru

ARUSHA&DODOMA VINARA UKUSANYAJI WA MAPATO

OR-TAMISEMI

**Ukusanyaji wa Mapato
Robo ya kwanza 2018/19**



www.tamisemi.go.tz

TC(Sh bilioni 1.07).

Jafo alizitaja halmashauri 23 zilizofanya vibaya ikianzia nay a mwisho kabisa kuwa ni Masasi Dc yenye asilimia 2 (Sh milioni 59.3), Nanyamba TC iliyokusanya Sh milioni 63,75 na Nanyumbu Dc Sh milioni 95.36(sawa na asilimia 3), Newala DC sh milioni 68.19 na Tandaimba Dc Sh milioni 211.6(sawa na asilimia 4).

Alizitaja zilizofikia makusanyo kwa asilimia 5 ni Songea DC(Sh milioni 83.9), Madaba DC (Sh milioni Sh milioni 38.1), Rory (sh milioni 99.9), Morogoro Dc (sh milioni 127.33), Namtumbo DC(sh milioni 153) huku zilizokusanya kwa asilimia 6 ni Tunduru Dc (Sh milioni 184.6) na Msalala Dc (Sh milioni 312.24).

Jafo alizitaja Halmashauri zilizokusanya kwa asilimia 7 ya makisio yao kuwa ni Mlele Dc (milioni 59), Nyasa Dc (sh milioni 93.98), na zile zilizokusanya asilimia 8 ya makisio kuwa

ni Nsimbo Dc (Sh milioni 87), Newala TC (Sh milioni 212), Bumbuli DC (Sh milioni 84.32), Kigoma Dc (sh milioni 56.3) na Mafia Dc (Sh milioni 129.5).

Jafo alitaja zilizokusanya kwa asilimia 9 ya makisio ya makusanyo yao kuwa ni Masasi TC(Sh milioni 275.25), Nyan-g'hwale Dc(Sh milioni124), Uvinza DC (milioni 152.86), na Momba Dc(Sh milioni 120).

Kwa upande wa Mkoa, Jafo alisema mikoa iliyofanywa vizuri na ikiongozwa na Mkoa wa Simiyu iliyofikisha asilimia 29 na mingine ni Manyara (asilimia 28), Lindi (asilimia 28), Mara (asilimia 24), Pwani (asilimia 23), Arusha (asilimia 23), Njombe (asilimia 22), Dodoma (asilimia 22), Mwanza (asilimia 21) na Geita (asilimia 21).

Jofo alitaja mikoa iliyofanywa vibaya kuwa ni Mtwara iliyokusanya kwa asilimia 6, Ruvuma kwa asilimia 11 na Kigoma kwa asilimia 13.

Aidha, Jafo alitumia fursa hiyo kumbusha viongozi wanaohusika kuwa ukusanyaji wa mapato wakiwamo wakurugenzi kuwa suala la mapato ndio kigezo ya kupimwa utendaji kazi wao.

Serikali imeanza mpango wa ku-karabati vituo vyote vya afya ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora na za uhakika kila wakati. Mpango mkakati wa kuboresha huduma za afya katika mikoa na mam-laka za Serikali za Mitaa, umeandaliwa kutokana na matokeo ya ziara iliyofany-wa na aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu Afya, Dk. Zainabu Chaula katika mikoa ya Tabora, Shinyanga, Mtwara na Lindi.

Kupitia ziara hiyo Dkt. Chaula alifanya kikao kilichohusisha Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Wizara ya Fedha na Mipango na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, na taasisi mbili ambazo ni Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na Bohari Kuu ya Madawa (MSD).

Akizungumzia mkakati huo, Dk. Chaula anasema anatambua juhudi na mchango wa idara na vitengo vilivyoko Ofisi ya Rais (TAMISEMI).

Anasema Serikali imedhamiria kwa dhati kutatua changamoto zinazowakabili wananchi, ikiwamo kuboresha huduma za afya katika maeneo yote.

“Sera, mikakati, miongozo na mipango mbalimbali iliyopo inalenga kusogeza huduma karibu na wananchi, ikiwamo Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (MMAM, 2007/17) na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi 2015, inaelekeza kusogeza huduma bora kwa wananchi zenye kufikika kwa urahisi wakati wote.

“Mojawapo ya viashiria vya huduma bora za Afya ni kutokuwapo au kuwapo idadi ndogo (tarakimu moja) ya vifo vya akina mama vitokanavyo na uzazi. Takwimu zinaonyesha mwaka 1996 kulikuwa na vifo vitokanavyo na uzazi 529 kwa kila vizazi hai 100,000, mwaka 2005 vifo vili-ongezeka na kufikia vifo 578/100,000,”anasema Dk. Chaula.

Anasema malengo yaliyowe-kwa na MMAM mwaka 2007, yalikuwa kupunguza vifo kutoka 578/100,000 hadi kufikia 175/100,000 ifikapo mwaka 2017.

Anasema malengo haya hayakuweza kufikiwa kwani takwimu za mwaka 2015/16, zinaonyesha uwapo wa vifo 556/100,000 (TDHIS, 2015/2016).

Anasema Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto kwa ku-shirikiana na wadau wa maendeleo wameandaa mpango mkakati unao julika-na kama Mpango Mkakati wa Taifa wa Pamoja (II) wa ku-punguza vifo vya akinamama na watoto (2016 – 2020).

Anasema moja ya mikakati iliyowekwa ni kuboresha huduma za afya ngazi ya msingi ambako ndiko walipo wananchi wengi. “Malengo yaliyowekwa na nchi ni ifika-po mwaka 2020 vifo vipun-gue hadi kufikia vifo 292/100,000 (One Plan II, 2016),”anasema Dk. Chaula.

Anasema makubaliano ya Kimataifa ya Malengo ya Maendeleo Endelevu (Sustainable Development Goals - SDGs) ambayo nchi wanachama zimeingia ikiwa-mo Tanzania, yanazitaka nchi hizo kupunguza vifo hadi kufikia vifo visivyozi-di 70/100,000 ifikapo mwaka 2030. Kwa hali ilivyo sasa sio rahisi kufikia malengo haya bila kuwa na mipango madhubuti .

Anasema Ofisi ya Rais

MAPINDUZI

TAMISEMI, ina jukumu la kusimamia Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa katika sera ya ugatuaji wa madaraka, ikiwa ni pamoja na kutafsiri na kutekeleza sera, miongozo na mipango mba-limbali katika uendelezaji mi-ji, usafiri, maji, afya na mazingira.

Anasema imedhamiria kwa dhati kusimamia maboresho ya hudu-ma za afya kwa kufanya mchanganuo wa kina na kuandaa mpango mkakati wa utekelezaji uliofanyiwa kazi na wizara nne. Anasema mpango wa MMAM, 2007/17), umeelekeza kuwa na zahanati kila kijiji na kituo cha afya katika kila kata.

Anasema mpaka sasa kuna za-hanati 6,640 sawa na asilimia 53, kati ya hizo, za Serikali ni 4,554 sawa na asilimia 36 katika vijiji 12,545. Anasema vituo vya afya vilivyopo ni 695 sawa na asilimia 15.7 ambapo vya Serikali ni 513 sawa na asimilia 11.6 tu kati ya kata 4,420 zilizopo .

“Miundombinu ya majengo ili-yopo ni michache isiyotosheleza mahitaji ya huduma, ikiambatana na changamoto nyingine za uchache wa rasilimali fedha, watu na vitendea kazi,”anasema Dk. Chaula.

Anasema kati ya vituo vya afya 513 vilivyopo, 115 sawa na asilimia 22.4 tu ndiyo vinatoa huduma za dharura na upasuaji pindi zinapohitajika. Ni dhahiri hudu-ma za afya bado zinahitaji ma-boresho makubwa kwa ku-shirikiana na wadau wote wali-opo.

KATIKA SEKTA YA AFYA



Naibu Katibu Mkuu OR-TAMISEMI anayeshughulikia afya

Dkt. Zainabu Chaula

“Huduma hii, inatolewa katika zahanati na vituo vya afya. Ngazi inayofuata ni ya hospitali za wilaya na mikoa (Secondary Health Care) na ngazi ya mwisho ni ya hospitali za kanda na Taifa (Tertiary Health Care). Huduma za afya katika ngazi ya msingi na sekondari zinanasimamiwa na ofisi ya TamiseMI, wakati zile za ngazi ya kanda na Taifa zipo chini ya usimamizi wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, ingawa kwa mujibu wa mfumo wa utoaji huduma nchini, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto ndiyo yenye dhamana ya kusimamia ubora wa huduma za Afya ikiwa ni pamoja na utungaji wa sera, miongozo na mipango mikakati.

Anasema kutokana na uchache wa vituo vya kutolea huduma za afya, watu wanasafiri umbali mrefu kutafuta huduma na kusababisha kero kwa wananchi katika maeneo

yenye vituo vya afya vichache na kuna halmashuari ina kituo cha afya kimoja tu kati ya kata 15. Hivyo wagonjwa hulazimika kusafiri kilomita zaidi ya 100 kutafuta huduma hizo ambazo bado pia haziridhishi.

“Kutokana na hali hii, wagonjwa wengi hubaki nyumbani au kuamua kwenda kwenye hospitali za wilaya, mikoa hadi Taifa ili kutafuta huduma hizo kwa gharama za juu. Hii inasababisha kuchelewa kupata huduma na kusababisha vifo au kulazwa hospitali kwa muda mrefu, lakini pia kuongeza mrundikano wa wagonjwa na watoa huduma kushindwa kumudu hali hiyo na kupelekea manung’uniko pande zote,” anasema

MKAKATI WA MABORESHO

Ili kutimiza lengo la kuboresha huduma za afya ya msingi, Dk. Chaula anasema ofisi ya Rais-TAMISEMI, imedhamiria kufanya ukarabati wa miundombinu ya kutolea huduma kwa viwango vya ramani zilizoidhinishwa na wizara husika.

Anasema kati ya vituo vya afya 513, ni 115 tu ndio vinatoa huduma ya dharura na upasuaji kwa mama mjamzito. Hivyo ukarabati utahusu vituo 398 ili kuviwezesha kutoa huduma ya dharura na upasuaji.

Mpaka sasa fedha zilizopatikana ni za ukarabati wa vituo 242. Pili, anasema kukamilisha maboma yote ifikapo 2020, maboma mengine yana zaidi ya miaka 10. Kuna maboma 1,845 yanayohitaji Sh bilioni 934, ikiwamo ukamilishwaji wa ujenzi wa hospitali za rufaa za mikoa na halmashauri.

Anasema mkakati wa tatu, ni kujenga vituo vya afya na zahanati maeneo ya mbali, angalau vituo 592 hasa kwenye halmashauri zisizo na kituo hata kimoja ili ifikie asilimia 25 ya mahitaji na zahanati 1,719 ili kufikia asilimia 50 ya lengo la kuwa na zahanati kila kijiji ifikapo 2025.

“Ujenzi wa kituo cha afya kipyaa, unahitaji shilingi bilioni 2.25 na ujenzi wa zahanati mpya unahitaji shilingi milioni 264, bila gharama za vifaa na vifaa tiba.

Kuhusu shughuli ambazo zimekwisha anza kutekelezwa, Dk. Chaula anasema Serikali imetenga Sh bilioni 69.9 katika bajeti ya mwaka wa fedha 2017/18 kwa ajili ya ukarabati, ujenzi wa hospitali 106, vituo vya afya 430 na zahanati 2,196.

Inaendelea Uk 22

MAPINDUZI KATIKA SEKTA YA AFYA

Inatoka Uk... ..21

“Pamoja na fedha hizi, Tamiseemi kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Wizara ya Fedha na Mipango na wadau wa maendeleo imeweza kupata fedha kwa ajili ya kuanza ukarabati na ujenzi wa vituo vya afya 246, zahanati 32 na umaliziaji wa majengo ya hospitali sita.

Anasema sambamba ujenzi wa vituo hivyo, fedha hizo pia zitatumika kununua vifaa tiba na kusimika Mifumo ya kielektroniki kwa ajili ya ukusanyaji wa taarifa.

“Tayari shilingi bilioni 22 zimetumwa tangu septemba, 2017 kwa ajili ya ukarabati wa vituo vya afya 44 na ukarabati unaendelea. Katika idadi ya vituo vya afya 246 vilivyo katika mpango wa ukarabati na ujenzi, vituo vya afya vinne vipya vitajengwa.

Anasema kuwa wastani sh milioni 500 zinaweza kufanya ukarabati mkubwa kwa kutumia “Force Account” na sh milioni 350 kununua vifaa na vifaa tiba.

Ukarabati na ununuzi wa vifaa na vifaa tiba kwa kituo cha afya ni Sh milioni 850, wakati zahanati ni Sh milioni 100, ikiwamo ununuzi wa vifaa tiba.

“Juhudi kubwa na endelevu zinahitajika za kutafuta fedha kwa ajili ya mabadiliko makubwa kwenye sekta hii,” anasema Dk. Chaula.



Uboreshaji wa miundombinu ya Afya katika kituo cha Afya Kahangara, Halmashauri ya Wilaya ya Magu



Uboreshaji wa miundombinu ya Afya katika kituo cha Afya Iyenze, Halmashauri ya Mji wa Kahama

Anasema shughuli zingine zinazoendelea sasa ni kusimamia utendaji bora wenye matokeo kupitia weledi, uwajibikaji na uadilifu wa pamoja, kuajiri watumishi kada mbalimbali wenye ujuzi 15,000 kwa mwaka wa fedha 2017/18 na kibali cha ajira mpya 2,554 tayari kimetolewa kufidia nafasi za watumishi walio simamishwa kutokana na sababu mbalimbali.

“Tumedhamiria kupeleka mafunzo ya mwaka mmoja wataalamu wa kutoa dawa za usingizi kwa ajili ya kuwezesha upasuaji kwenye vituo vya kutolea huduma 400, kuboresha utunzaji na matumizi ya takwimu kwa kutumia mifumo ya (GOTHOMIS) na “Planrep” ili-yoboreshwa amesema Dk. Chaula.

Anasema mkakati mwingine, ni kuanzisha mzabuni mshitiri (Prime Vendors) na “Drug Revolving” Fund (DRF) nchi nzima ili kuhakikisha upatikanaji wa dawa ni wa uhakika kwa asilimia 100 wakati wote, kudhibiti makusanyo ya mapato katika vituo vya huduma na kupeleka fedha moja kwa moja vituoni, ikiwa ni pamoja kuajiri wasaidizi wa hesabu 535 kwenye vituo vya afya (tayari wapo vituoni), kuhimiza malipo kwa kadi.

Ujenzi wa kituo cha afya kipya, unahitaji shilingi bilioni 2.25 na ujenzi wa zahanati mpya unahitaji shilingi mil. 264 – Dk. Chaula.

WATUMISHI TAMISEMI WASHIRIKI MAANDAMANO YA AMANI KUMPONGEZA JPM

Wafanyakazi wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa wameshiriki maandamano ya amani ya kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa kurudisha kikokotoo cha awali kwa mafao ya wafanyakazi.

Katika maandamano hayo Wafanyakazi wote nchini wametakiwa kufanya kazi kwa bidii na kujituma ili kuleta chachu ya ufanisi katika kutekeleza kazi zao.

Hayo yamebaishwa na Waziri Mkuu Wa Jamhuri Ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa ambaye alikuwa mgeni rasmi katika maandamano hayo ya amani.

Mhe. Majaliwa amesema kuwa tarehe 3 Januari 2018 bunge lilipitisha muswada wa sheria wa kuunganishwa kwa mifuko minne ya pensheni na kuifanyia marekebisho sheria ya NSSF lengo ni kupunguza gharama za uendeshaji wa mifuko hiyo.

Aidha, Mhe Majaliwa amesema katika kujali maslahi ya wafanyakazi Mh Magufuli alisema vikokoto vilivyokuwa vinatumika awali virudishwe katika kipindi hiki cha mpito, huku mjadala wa kusuburia kupata muafaka wa kikotoo sahihi kitakachotumika.

“Kikubwa niutake uongozi wa Wafanya kazi Nchini kushirikiana na mamulaka husika ili kuhakikisha wafanyakazi wanapata huduma bora kutoka katika mifuko hii” Amesema Majaliwa

Kwa upande Waziri mwenye dhamana ya sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira Na Walemavu Mh Jenista Muhagama amesema kuwa hivi karibuni ameanza kutilia mkazo maagizo na maelekezo ya Mhe Rais Magufuli huku wakifanya zoezi la kukagua Mikoa yote ili kuhakikisha watendaji wa mifuko ya kijamii hawapotoshi maagizo hayo.



Watumishi wa OR-TAMISEMI wakishiriki maandamano ya amani yaliyofanyika Jijini Dodoma

Naye katibu mkuu wa chama cha wafanyakazi TUC-TA ndugu Yahya Msigwa amesema amempongeza Rais Magufuli kwa kusikiliza kilio chao, zoezi ambalo limeanza tangu mwaka 2008 na kuamuru mchakato wa kuunganishwa mfuko kuanze mara moja.

“Lengo lakuomba kuunganisha mifuko ni kupunguza ghalama za uendeshaji, kudhibiti matumizi mabaya ya fedha katika mifuko hii na kuondoa hali ya kugombania wanachama wa mifuko na kuifanya kama biashara” Amesema Msigwa.

Ikumbukwe mwishoni mwa mwaka jana 28 Disemba 2018, Rais Magufuli alikutana na viongozi wa vyama vya wafanya kazi nchini na kujadili masilahiya mafao yao na mwisho wa kikao hicho aliamua kikokotoo kibaki kama kilivyo kuwa awali mpaka hapo mbadala utakapo patikana 2023.

OFISI ya Rais Tawala za mikoa na Serikali za mitaa (TamiseMI) imebaini matumizi mabaya ya fedha za serikali Sh. bilioni 2.98 katika halmashauri ya Ulanga mkoani Morogoro na kuagiza wakuu wa idara wote waliohusika wavuliwe nyadhifa zao huku watumishi wengine waondolewe majukumu ili vyombo vya dola viendeleo na hatua kwa mujibu wa sheria dhidi yao.

Hayo yamebainishwa na Waziri wa nchi ofisi ya Rais Twala za mikoa na Serikali za mitaa Mhe. Selemani Jafo wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari juu ya uchunguzi maalum uliofan- ywa kwa halmashauri ya wilaya hiyo.

Jafo alisema kuwa Ofisi ya Rais TamiseMI imefanya uchunguzi maalum katika halmashauri 12 nchini ambazo ni Ulanga, Same, Mbulu, Meru, Itigi, Misungwi, Nyang'hwale, Serengeti, Bahi, mpwapwa, Morogoro Dc na Kibaha Tc ambapo katika halmashauri ya Ulanga uchunguzi ulianza Novemba 13 hadi 23 mwaka huu.

Alisema uchunguzi huo ulifanyika kufu- atia malalamiko ya wanachi mbalimbali pamoja na mbunge wa jimbo la Ulanga Mhe. Goodluck Mlinga kutokana na ubadhirifu uliokuwepo.

Aidha alisema kiasi hicho kimebainika kupotea kutokana na matumizi mabaya ya fedha za serikali ambapo watumishi wasio waadilifu katika halmashauri hiyo walikiuka taratibu na kufanya manunuzi hewa na kutumia vibaya fedha kinyume na malengo yaliyopangwa .

"Halmashauri hii imekuwa ikifanya udanganyifu katika taarifa za miradi ya maendeleo taarifa za mfuko wa wana- wake na vijana, kwa ujumla inausimamizi mbovu wa mapato na kuwa na udhibiti hafifu wa makusanyo na matumizi ya fedha za Umma"alisema Jafo.

Jafo alisema kuwa mkurugenzi mtendaji

Wa Halmashauri ya Ulanga Yusuph Daud Senguruka kwa nafasi yake ya afisa masuhuli alishindwa kusiomamia sheria ya fedha za serikali za mitaa katika kudhibiti na kuweka mifumo dhab- iti ya kuhakikisha fedha ziko salama kuanzia ma- kusanyo hadi matumizi yake.

"Hii ni pamoja na kushindwa kumsimamia mweka hazina wa hal- mashauri katika ku- tekeleza majukumu yake na kwa kushindwa ku- tekeleza majuku hayo amesababisha hasara halmashauri ya shilingi 2,980,172,763.60"alisem a Jafo.

Alifafanua kuwa Rajabu Siriwa, ambaye alikuwa ni mweka hazina wa hal- masahuri hiyo alichangia kuhujumu mapato ya serikali kwa kuweka utaratibu ambao umeisababishia hasara serikali .

Alisema kuwa mweka hazina huyo aliidhinisha malipo ya sh. 225,586,400 nje ya bajeti bila idhini ya ofisi ya Rais TamiseMI ambapo malipo hayo yalikusishwa posho ya safari ya mku- rugenzi mtendaji Sh. 192,000,000.

"Pia kukusanya mapato na kutoyapeleka benki, katika mfumo wa LGR- CIS umeonyesha hal- mashauri ilikusanya fedha ambazo

"Halmashauri hii imekuwa ikifanya udanganyifu katika taarifa za miradi ya maendeleo taarifa za mfuko wa wanawake na vijana, kwa ujumla inausimamizi mbovu wa mapato na kuwa na udhibiti hafifu wa makusanyo na matumizi ya fedha za Umma" - Waziri wa Nchi, OR- TAMISEMI, Mh. Selemani Jafo

hazikupeleleka benki kabisa shilingi 760,686,732.43 fedha hizi hazijulikani matumizi yake halisi ni nini"aliohoji Jafo.

Aidha alisema kuwa mweka hazina huyo aliandaa taarifa zenye udanganyifu kwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayotumia fedha za makusanyo ya ndani.

"Halmashauri imeripoti kupeleka shilingi 301,442,686 uhalisia wamepeleka 113,406,106.34 na udanganyifu katika mfuko wa vija- na na akina mama halmashauri inaripoti kupeleka shilingi 120,000,000 uhalisia wamepeleka sh. 31,500,000 kwa mwaka 2017/18 na 2018/19 hadi novemba 2018 wakati uchunguzi unakamili- ka"alisema

Aidha Jafo alisema kuwa Mhandi- si David Kaijage akiwa anakaimu ofisi ya Mkurugenzi februari mosi mwaka huu hadi februari nne ali- husika kwenye kuihujumu hal- mashauri kwa mapato ya Sh. 470,000,000 yaliyopolelewa kuto- ka kiwanda cha kilombero Valley Teak Company

WATUMISHI 13 ULANGA HATIANI UBADHIRIFU WA BIL 2.9



**Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
Mhe. Selemani Jafo (Mb)**

kwa kuzirejesha kwa mlipaji siku hiyohiyo waliyopokea.

"Pia alisaini hati ya malipo kumlipa bahari Phamarcy kwa siku ambayo hakuwa kaimu mkurugenzi na mkurugenzi alikuwepo" alisema.

Wakati huo huo Bw. Stanley Godwil Nyange na Bw. Isaack Mwasankope Salumu ambao wote ni wahasibu wameihujumu Halmashauri kwa kutumia akaunti zao binafsi kupokea fedha za makusanyo ya Halmashauri kiasi cha sh 203.398,700 aliongeza.

Waziri Jafo pia alisema kuwa uchunguzi huo pia umebainisha kuwa Isaack Mwasankope, Salehe Mbogoso pamoja na Johson Mwanyombole

ambao wote ni wahasibu wa halmashauri hiyo walihusika kuchukua fedha taslim za makusanyo katika kituo cha kuvukoni na kisha kuzitumia bila kuzipeleka Benki sh 168,000,000.

Yassin Galahenga na Mohamed Majaliwa Saidi wataalam wa mifumo (TEHAMA) walishirikiana na wahasibu kurekebisha Ankara na kufuta madeni bila idhini ya Mkurugenzi alibainisha Waziri Jafo.

Waziri Jafo aliongeza kuwa Bw. Willy Ndabila ambaye alikuwa

alikuwa afisa manunuzi alihusika na manunuzi hewa ya madawa yenye thamani y ash. 73,212,909.40 pamoja na kulipa fedha zaidi yaani sh 146,425,818 huku Goodluck Mbata ambaye ni muhasibu wa hospital aliandaa malipo na kusainisha mara mbili kwa watu tofauti huku akijua kufanya hivyo ni kuandaa malipo mara mbili kwa hitaji moja .

Waziri Jafo aliagiza ofisi ya mkuu wa mkoa wa Morogoro kuhakikisha kuwa wakuu wa idara na vitengo waliohusika akiwemo Willy Ndabila ambaye amehamishiwa itilima, na Rajabu Siriwa ambaye amehamishiwa Gairo wavuliwe nyadhifa zao na mamlaka za nidhamu na vyombo vya dola viendeele na hatua kwa mujibu wa sheria.

Aliongeza kuwa watumishi wote waliohamishiwa Halmashauri ya ulanga wakiwa na makosa yaani DPMU Willy Ndabila na DT Rajabu Siriwa warejee Ulanga ili kuiwezesha halmashauri na vyombo vya Dola kufanya kazi yake. "Maelezo juu ya mkurugenzi huyu wa Ulanga yenyewe yatatolewa baadaye na serikali" alifafanua Jafo.

Hata hivyo Jafo alisema kuwa mkuu wa mkoa wa Morogoro ahakikishe kuwa Ofisi ya Rais Tamiseemi imepata maelezo kwani wataalamu hao hawakuchukuliwa hatua stahiki zenye tija dhidi ya taarifa za mkaguzi wa ndani ya robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2017/18 kabla ya januari 15 2019.



OFISI YA RAIS
TAMISEMI

MAWASILIANOTAMISEMI



Mhandisi. Joseph Nyamuhanga

Katibu Mkuu - Ofisi ya Rais TAMISEMI

Tunakupongeza kwa kuteuliwa kushika nafasi ya Katibu Mkuu - Ofisi ya Rais TAMISEMI. Tunakuhidi Ushirikiano wa kutosha katika utekelezaji wa majukumu yako.

www.tamiseemi.go.tz

Kwaheri &



OFISI YA RAIS
TAMISEMI

MAWASILIANOTAMISEMI



Dkt. Zainabu Chaula

Tunakupongeza kwa kuteuliwa kushika nafasi ya Katibu Mkuu (anayeshughulikia Afya) katika Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

Kila la Kheri

www.tamiseemi.go.tz

#KwaheriTAMISEMI

Karibuni Viongozi



Dkt. Dorothy Gwajima

Naibu Katibu Mkuu (Afya) - Ofisi ya Rais TAMISEMI

Tunakupongeza kwa kuteuliwa kushika nafasi ya Naibu Katibu Mkuu (Afya) - Ofisi ya Rais TAMISEMI. Tunakuahidi Ushirikiano wa kutosha katika utekelezaji wa majukumu yako.

www.tamiseemi.go.tz

#KaribuTAMISEMI



Kila la Kheri Mhe. Kakunda

Kwa pamoja tunakupongeza kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

www.tamiseemi.go.tz

#KilalaKheriGKakunda



OFISI YA RAIS
TAMISEMI

MAWASILIANOTAMISEMI



Mhe. Mwita M. Waitara
Naibu Waziri TAMISEMI

Karibu OR TAMISEMI

Kwa pamoja tunakupongeza kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI. Tunakuahidi ushirikiano wa kutosha katika utekelezaji wa majukumu yako.

www.tamiseemi.go.tz

#KaribuTAMISEMI



OR-TAMISEMI

www.tamisemi.go.tz